

Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

112

SANAA ZA UBUNIFU NA MICHEZO

MUDA: SAA 2:30

JUMATANO 16 OKTOBA, 2024 MCHANA

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Jibu swali MOJA (1) kutoka sehemu C.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Tumia kalamu nyeusi au ya buluu kwa kuandikia na michoro iwe kwa penseli.
6. Simu ya mkononi na vituvisivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



0122477

Mtihani huu una kurasa 10 zenye maandishi

**SEHEMU A: (Alama 35)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi yake kwenye jadweli lililopo hapo chini.
  - i. Kinywaji kipi kinachopendwa sana wakati wa joto?
    - A. Chai
    - B. Maji
    - C. Maziwa
    - D. Uji
  - ii. Neno viamba upishi lina maana ya
    - A. Vifaa vinavyotumika wakati wa kupika
    - B. Vitu mbali mbali vya kupikia
    - C. Viungo vinavyohitajika katika upishi
    - D. Viungo vya upishi vyenye asili ya vimiminika
  - iii. Moja kati ya misingi ya ujasiriamali ni
    - A. Kutumia vibubu
    - B. Masoko
    - C. Matumizi ya fedha
    - D. Viwanda
  - iv. Njia kuu ya kutafuta mtaji wa biashara ni
    - A. Akiba binafsi ya fedha
    - B. Kufanya magendo
    - C. Kununua viwanja
    - D. Kuwa na marafiki
  - v. Mapumziko katika michezo ni jambo muhimu. Ni yepi madhara ya kutokupumzika katika michezo?
    - A. Kucheza kwa ufanisi
    - B. Kupata hamu ya kucheza
    - C. Kuongeza uwezo wa kufikiri
    - D. Kupata maumivu mwilini

## Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

- vi. Mashindano huru ya uogeleaji yanahitaji masafa yenye urefu wa
- A. Kilomita 3
  - B. Kilomita 4
  - C. Kilomita 5
  - D. Kilomita 10
- vii. Moja kati ya zifuatazo ni dalili ya mtu aliyevunjika
- A. Ngozi kupiga wekundu eneo husika
  - B. Kukauka kwa damu mwilini
  - C. Kutokwa na jasho jingi
  - D. Kutembea sawa sawa
- viii. Miongoni mwa hatua muhimu katika kuibua igizo ni kuwa na
- A. Dhana
  - B. Jukwaa
  - C. Waigizaji
  - D. Wasanii
- ix. Moja kati ya vifaa vifuatavyo hutumika kukatia vigogo vya miti
- A. Kisu
  - B. Kwanja
  - C. Mkasi
  - D. Shoka
- x. Miongoni mwa njia bora za kisasa za kuhifadhi chakula kibichi ni
- A. Kukaanga
  - B. Kukausha
  - C. Kutia chumvi
  - D. Kutia kwenye friji

### JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Oanisha maelezo kutoka **KIFUNGU A** kwa kuchagua jawabu sahihi kutoka **KIFUNGU B** kama yanavyotumika katika mada ya kuogelea. Andika herufi Kwenye jadweli hapo chini.

<b>KIFUNGU A</b>	<b>KIFUNGU B</b>
i. Kutazama mazingira ya sehemu ambayo mtu amezama.	A. Boya la uokozi
ii. Likivaliwa humfanya mtu aelee katika maji	B. Kamba
iii. Kifaa chenye umbo la duara ambacho hurushiwa mtu aliezama ili akishike na kuelea	C. Koti la uokozi
iv. Kifaa ambacho hutumika endapo kuna dharura ya meli kuzama.	D. Kuogelea
v. Hali ya mtu kuishiwa pumzi na nguvu katika maji	E. Kuzama
	F. Mbinu ya uokozi
	G. Rafti ya kuokolea maisha

**JAWABU**

<b>ORODHA A</b>	i.	ii.	iii.	iv.	v.
<b>ORODHA B</b>					

3. Andika herufi **K** kwa maelezo yaliyokuwa sahihi na herufi **S** kwa maelezo yasiyokuwa sahihi katika jadweli lililopo hapo chini.
- Ujasiriamali huongeza umaskini katika jamii.
  - Kala linalotumika kubania nywele huweza kutengenezwa kwa kifuu.
  - Mtaji ni kiwango cha fedha ambacho mjasiriamali huanzia biashara.
  - Baadhi ya vyakula hupikwa kwa kuokwa.
  - Jinzi na kilemba ni nguo zinazofaa katika kuogelea.
  - Madhara ya kutohifadhi mazingira ni kupungua kwa mvua nchini.
  - Mashairi ya kimamboleo ni mashairi ambayo huzingatia urari wa vina na mizani.

## Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

- viii. Huduma ya kwanza ni somo linalotufundisha namna ya kula na kunywa kwa maelekezo ya daktari.
- ix. Mfupa wa mtoto uliovunjika huona haraka ukilinganisha na wa mtu mzima.
- x. Miongoni mwa dhima za mashairi ni kuelimisha jamii.

### JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye sanduku lililopo chini.

kibaskeli,	mazingira,	melodrama,	landa,
kinywaji,	kiubavuubavu,	msumeno	

- i. Kimiminika ambacho binadamu hukitumia kwa manufaa ya mwili wake huitwa \_\_\_\_\_
- ii. Kifaa ambacho hutumika kusafishia mbao huitwa \_\_\_\_\_
- iii. Tamthilia inayohusisha wimbo, ngoma au muziki huitwa \_\_\_\_\_
- iv. Vitu vyote vilivyotuzunguka ikiwemo miti na wanyama hujulikana kama ni \_\_\_\_\_
- v. Mtindo wa kuogelea ambapo muogeleaji huelea huku miguu na mikono ikipishana katika mtindo wa kupokezana huitwa \_\_\_\_\_

**SEHEMU B: (Alama 45)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

5. a) Ainisha sababu tano (5) za unyanyasaji wa kijinsia.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_
- iv. \_\_\_\_\_
- v. \_\_\_\_\_

b) Taja aina nne (4) za unyanyasaji wa kijinsia.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_
- iv. \_\_\_\_\_

6. a) Andika mambo matatu (3) ya kuzingatia ili kumudu usafi wa jikoni.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_

b) Orodhesha vyakula vitatu (3) vinavyopikwa kwa kutumia chumvi.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_

7. a) Elezea maana ya mfanyabiashara.

---

---

---

b) Bainisha hatua tatu (3) za kuandaa misingi ya ujasiriamali.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_

8. a) Kapungulo alikuwa mchezaji bora wa timu ya taifa ya Kusadikika lakini kiwango chake kilishuka kutokana na utumiaji wa dawa zisizokubalika. Bainisha madhara matano (5) ya kutumia dawa za aina hiyo.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_
- iv. \_\_\_\_\_
- v. \_\_\_\_\_

b) Taja faida nne (4) za lishe bora kwa mwanamichezo.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_
- iv. \_\_\_\_\_

9. a) Eleza kwa ufupi maana ya kujitambua.

---

---

---

---

b) Taja faida tatu (3) za kujitambua.

- i. \_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_
- iii. \_\_\_\_\_





**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]











